



**TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO TANZANIA
(TARI)**

TARI RIC3 (TXD307)

**MBEGU BORA YA MPUNGA
YENYE MCHELE
ANGAVU**



@Tari tv



@Tari Tanzania



@tari tv

UTUNZAJI WA ZAO SHAMBANI

Upandaji– Panda au pandikiza
kwa mistari shambani

Nafasi-shina kwa shina sm 20,
mstari kwa mstari sm 20

Mbolea ya kupandia – Tumia NPK
au DAP kwa viwango vilivyo
shauriwa kitaalamu

Mbolea ya kukuzia – Weka mbolea
ya kukuzia kwa awamu mbili, Awamu
ya kwanza siku 14 baada ya
kupandikiza na awamu ya pili mpunga
unapofikia umri wa siku 55 baada
ya kuota kitaluni

Mbolea za majani – Tumia mbolea za
kupulizia kwenye majani kulingana
na ushauri wa kitaalamu

Kuvuna – Vuna kwa wakati na kausha
mpaka 14% ya kiwango cha unyevu
kwa ukobokaji mzuri na hifadhi ya
muda marefu

SIFA ZA MBEGU

Inafaa kwa kilimo cha umwagiliaji
na mabondeni

Inastawi ukanda wa chini na
wakati(mita 100 – 1,200) kutoka ,
usawa wa bahari

Mavuno ni kati ya tani 6.5 hadi 7.0
kwa hekta Urefu wake ni
sentimita 100


Ina mashina imara, haianguki
shambani

Inastahimili magonjwa na wadudu

Inakomaa kwa siku 120 hadi 125

Inazaa masuke mengi

Ni rahisi kupiga



SIFA ZA MPUNGA



- Unakoboleka vizuri, 65 – 70% mchele
- Una muonekano mzuri
- Mpunga una punje ndefu
- Punje zake ni nzito

Sifa za Mchele

- Mchele wake unanukia vizuri
- Punje zake ni nzito
- Mchele wake ni angavu zaidi na wenye ubora wa juu sokoni

Sifa za Wali

- Unanukia vizuri
- Una ladha nzuri, mtamu
- Hubakia laini, hata baada ya kupoa unafaa kula





**Mbegu inayonukia
na yenye mavumo mengi
kwa kilimo cha
mabondeni na umwagiliaji**





**Kwa maelezo zaidi wasiliana na :
Meneja wa kituo
TARI Dakawa
S.L.P 1892, Morogoro, Tanzania
Simu: (+255) 23 2934300,
Baruapepe: cmdakawa@tari.go.tz**

**Kimetayarishwa na:
Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania
KITUO CHA DAKAWA**